MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.17: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya Machi 11 -20, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Machi 21-31, 2026*

**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitasaidia ukuaji wa mazao, hata hivyo wakulima wanashauriwa kuchukua tahadhari ya magonjwa ya mazao yasababishwayo na maji kutuama mashambani.
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wanashauriwa kuendelea na shughuli za palizi.
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao huku wakiendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2026


Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudpungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, kanda ya kati, kusini na nyanda za juu kusini magharibi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii ilipelekea kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi ya nchi. Pia, vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki na nyanda za juu kusini magharibi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2026

Katika dekadi hii, maeneo mengi nchini yalipata jumla ya mvua za siku kumi kati ya milimita 51 hadi 100, hali inayoonyesha kuwa mvua zilinyesha kwa usambazaji mzuri.

Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha kati ya milimita 151 na 200, kilirekodiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini (Tanga, sehemu za kaskazini za Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na pwani ya kusini (Mtwara na Lindi) kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 11-20, 2026

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2026

Katika dekadi hii, kiwango cha mvua kilichorekodiwa katika maeneo mengi ya nchi kimeboresha hali ya unyevu wa udongo na kwa ujumla kimesaidia katika ukuaji wa mazao, ingawa kumekuwepo na matukio ya maji kutuama katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Morogoro, Shinyanga na Mwanza.

Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya kwa mwaka, hususan ukanda wa pwani ya kaskazini, kanda la Ziwa Victoria na sehemu za nyanda za juu za kaskazini mashariki, wakulima wengi waliendelea shughuli za palizi. Mwenendo wa mvua unaendelea vizuri na umesaidia katika ukuaji wa mazao.

Katika mkoa wa Morogoro, zao la mpunga liko katika hatua ya kuchipua matawi. Ongezeko la mvua linaweza kusaidia katika ukuaji wa mpunga, hasusan katika mashamba ya umwagiliaji

Katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua, zao la mahindi liko katika hatua ya ukuaji wa majani, ingawa katika mkoa wa Tabora, mahindi yamefikia hatua ya ukomavu wa nta. Mkoani Dodoma, mazao ya alizeti na mtama yako katika hatua za awali za ukuaji.

Mazao ya kudumu kama kahawa, hasusan katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe, yako katika hatua ya tunda laini. Uwepo wa unyevu wa kutosha kwenye udongo umeendelea kusaidia ukuaji wa kahawa, hasusan katika hatua hii muhimu ya matunda.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori umeongezeka katika maeneo yaliyopata mvua za kutosha.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kiliongezeka kiasi hususan kwa maeneo ambayo yaliyokuwa na ongezeko la mvua.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuwepo katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo.

Aidha, upepo wa bahari wenye unyevunuevu unatarajiwa kuvuma kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani. Hali hii inatarajiwa kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya pwani ya nchi yetu na yale ya nyanda za juu za kaskazini-mashariki. Pia, mifumo ya hali ya hewa katika ukanda wa Ziwa Victoria inatarajiwa kuimarika, hali itakayochangia kuongezeka zaidi kwa mvua katika ukanda huo pamoja na maeneo yanayopakana hususan yaliyopo magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Maeneo ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Hali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itaongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa mazao.

**Ushauri:**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Hali ya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi inayotarajiwa zitasaidia katika ukuaji wa wa mazao na shughuli za palizi. Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini):** Mvua zinazotarajiwa katika maeneo haya zitasaidia ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kufuatlia hali ya mazao na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kudumishwa kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)